



# Nishani ya ujenzi wa moto na mapishi ya kambi (fire building and camp cookery).

Nishani hii ipo katika kundi la maburudisho na michezo, huwakilishwa kwa rangi ya kijani






By: Yusuph Mwasiposya

## Aina za mioto

Tengeneza aina tano za mioto ya kambi na uoneshe matumizi yake. Mioto miwili kati ya mioto hiyo ni lazima iwe ni ya kupikia chakula

1. **Hunter's fire (Moto wa mwindaji)**: katika moto huu magogo huwekwa karibu karibu na kuwa kama mafiga yanayoweza kubebe sufuria au kifaa kinginecho cha kupikia

- Matumizi makubwa ya moto huu ni kupikia



2

## Aina za mioto

2. **Reflector Fire (Moto wa kuakisi)**: moto huwashwa, kisha huchukuliwa kitu cha kurudisha joto(reflector) ili joto likifika kwenye reflector hiyo liweze kurudi tena lilikotoka. Reflector yaweza kuwa jiwe, magogo au bati

- Moto huu huweza kutumika kwa ajili ya kuokea ingwa si fanisi kama reflector oven
- Hutumika kuupa mwili joto wakati wa usiku au wakati wa baridi




3

## Aina za mioto

3. **Star Fire (Moto wa nyota)**: uzuri wa moto huu ni kwamba magogo yanaweza kuwa katika urefu wowote, hivyo kukwepa usumbufu wa kuyakatakata

- Hutumika kuupa mwili joto wakati wa usiku au wakati wa baridi



4

## Aina za mioto

4. **Teepee Fire**: Moto huu ndio unaongoza kwa matumizi tunapokuwa kambini(hasa kambi la moto). Utengenezaji wa moto huu una ugumu kidogo kuliko mioto mingine. Magogo husimamishwa, na kuegemeshwa kila mmoja na chini ya magogo hayo huwekwa kuni ndogo ziwezazo kushika moto kwa urahisi

- Hutumika kuupa mwili joto wakati wa usiku au wakati wa baridi (hasa wakati wa masimulizi na ikiwa kuna watu wengi katika eneo moja)



5

## Aina za mioto

5. **Log Cabin Fire**: moto huu ni rahisi kutengeneza na pia ni salama Zaidi, ingawa unahitaji magogo mengi kuliko teepee fire. Uwashaji wake ni mgumu kuliko teepee kwa sababu kuni ndogo huwa chini sana hivyo kumpa shida muwashaji, ingawa waweza kuwashwa kwanza na kisha magogo yakapangwa baada ya kuwashwa kwake




6

## Aina za mioto

**6. Council Fire**: moto huu ulitumika sana na wamarekani wa zamani wakati wa mikutano.

- Unapaswa kuwa makini unapoutengeneza moto huu kwa sababu unapaswa kuachia nafasi kidogo kati ya magogo ili kuruhusu mzunguko wa hewa na kusaidia moto kuendela kuwaka.
- Moto huu hutumia kuni nyingi sana.
- Wakati mwingine huitwa moto wa piramidi



7

## Aina za mioto

**7. Trench Fire**:

- Chimba mtaro wenye upana wa sm13, urefu wa kwenda chini sm17 – sm22
- Weka vimti vibichi toka upande mmoja wa mtaro hadi upande mwingine ili kusaidia kushika sufuria lako
- Moto huu hufaa sana sehemu zenye upepo, maana upepo haufiki moja kwa moja
- Lakini wakati wa mvua, mtaro hujaa maji haraka sana na kufanya moto uzime



8

## Aina za mioto

**8. Indian Fire**:

- Tengeneza teepee fire
- Zungushia magogo pembeni
- Uzuri wa moto huu ni kwamba huwaka kwa muda mrefu na hutoa mwanga na joto la kutosha, hii ni kwa sababu huchukua kuni nyingi



9

## Aina za mioto

**8. Backlog Fire**:

- Moto huu huwa badala ya council fire au log cabin fire ikiwa kambi lina watu wachache
- Tengeneza teepee fire kadhaa na kisha uziegemeshe kwenye gogo ili kufanya moto huu



10

## Aina za mioto

**8. Brush Fire**:

- Kata kuni kwa urefu unaolingana
- Rundika kuni kulingana na urefu wake kwa kuelekeza uelekeo wa upepo
- Tengeneza teepee fire kutoka upande ambao upepo hutokea kisha washa moto wako
- Uzuri wa moto huu ni kwamba huwaka sana na hauhitaji kuni nyingi sana, pia huwaka kwa muda mfupi
- Kuwa makini, usiwashe moto huu ikiwa kuna upepo mkali sana



11

## Viwashio vya moto

**Fuzz sticks**: hivi ni vijiti vyenye ncha nyingi kama brashi, ncha hizi zikishika moto haziwezi kuzima kwa urahisi mpaka moto ukolee

Utengenezaji

- Chukua kijiti chenye urefu wa kalamu na kisu kikali
- Anza kukata kijiti hicho kwa namna ya kuchubua, hakikisha vile unavyovikata visitoke kwenye kijiti
- Kata mara nyingi iwezekanavyo ili uongeze uwezekano wa kijiti kushika moto



12

## Namna ya kuwasha moto

a. **Kichochezi (Fuel)**: vichochezi vimegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni

- Tinder: hivi ni vitu ambavyo hushika moto kwa haraka sana, ni lazima view vikavu, vyembamba na view katika kiasi cha kutosha. Mfano wa tinder ni vijiti vya mpaina, nyasi kavu, majani ya mlingoti, karatasi au manyoya ya ndege
- Kindling: hivi ni vijiti ambavyo ni vikubwa kiasi, mara nyingi huwa na ukubwa unaolingana na ukubwa wa kalamu. Kindling hizi ndizo hukatwa ili kupata fuzz sticks kwa ajili ya kurahisisha uwashaji wa moto.
- Fuel (kichochezi): hizi ni kuni kubwa au magogo ambayo huwaka mara baada ya tinder na kindling kushka moto kiasi cha kutosha, vichochezi hivi ndivyo hufanya moto uendelee kuwaka

13

## Namna ya kuwasha moto

b. **Hewa (Air)**:

- Hewa ni lazima ili kuwasha moto wa aina yoyote
- Kuwa makini unapopanga kuni zako ili zisibabnane sana kiasi cha kuzuia hewa kuzunguka na kuufanya moto wako kuendelea kuwaka
- Wakati wa kuwasha moto hakikisha Hakuna upepo unaopiga moja kwa moja katika vifaa vyako vya kuwashia moto, ikiwa sehemu hiyo ina upepo mwingi, jitahidi kutafuta namna ya kuuzuia

c. **Joto (heat):**

Moto huongezwa kwa kutumia kibiriti, kaa la moto au kifaa kinginecho chochote cha kuwashia moto

- Ikiwa utatumia nyia ya upekechaji kuwasha moto, ni lazima utenganishe tinder pembeni na zikishika moto ndipo uzipeleke kwenye kindling ili ziweze kukolea na kuwasha vichocheo kisha moto uendelee kuwa vema.
- Ili kufanya moto uzime, tengenisha kuni ili joto lake litawanyike, hivyo moto utashindwa kuendelea kuwaka

14

## Sheria za usalama wa moto

1. Weka moto mahali pasipo na nyasi au chochote cha kushika moto kirahisi na kuufanya usambae, inapendekezwa kuhakikishwa kuwa eneo liwe safi ndani ya mita 3 za kuzunguka eneo la moto
2. Usiwashe moto karibu na matawi ya miti yanayoning'inia
3. Washa moto bila kutumia vichochezi kama mafuta ya taa
4. Kabla ya kuondoka eneo hilo, hakikisha eneo ni safi kabisa na moto umezima kabisa na kubaki majivu
5. Usiwashe moto juu ya vitu viwezavyo kushika moto haraka na kuusambaza
6. Hakikisha vifaa vya kuzimia moto haviko mbali nawe wakati wote moto unapokuwa unawake
7. Usiondoe vijiti viwakavyo kutoka kwenye moto
8. Kuwa mwangalifu kwa vipande vya moto vinavyoruka kutoka kwenye moto, na hakikisha unavizima haraka sana
9. Funika miguu yako vizuri wakati wa kuota moto
10. Usichome vitu vinavyoweza kuelea vikiwa na moto ili kuzuia kusambaa kwa moto. Mfano karatasi
11. Usiwashe moto wakati wa upepo mkali ili kuzuia moto usije ukasambaa

15

## Sheria za matumizi ya shoka

1. Jifunze kutumia shoka kwa usahihi
2. Hakikisha Hakuna mtu aliye karibu na wewe wakati wa kukata kuni. Kukwa makini maana shoka laweza kuchomoka 2Falme 6:5
3. Unapochanja kuni hakikisha lile gogo linalochanjwa limewekwa juu ya gogo linguine ili kukurahisishia kazi
4. Shusha shoka lako katika eneo ambalo halitasababisha gogo ulilolikanyaga kubadilisha mkao, maana hii inaweza kukusababishia majeraha. Kuwa makini
5. Shika shoka lako kwa mikono yote miwili
6. Usiweke miguu yako sehemu moja wakati wa kupasua kuni

16

## Onyesha uwezo wako wa kuwasha moto kwenye mvua au mafuriko

1. Tafuta gogo na kisha ukukate katikati na kutoka hapo katikati toa viwashio vya moto
2. Tengeneza sehemu kavu kwa ajili ya kutunza kuni zako unazokusanya. Unaweza ukazikusanya juu ya turubai, na baada ya kuzikusanya ukazifunika na kuziwekea mawe ili zisiendelee kulowa
3. Andaa vema sehemu ya kuwashia moto
4. Hakikisha viwashio vvyako havina unyevunyevu, na usiviweke sehemu yenye unyevunyevu
5. Washa moto wako kwa uangalifu
6. Baada ya moto kukolea, unaweza kuweka kuni zenye unyevunyevu maana ikiwa moto ni mkali kiasi cha kutosha kuni hizo zitwaka vizuri

17

## Mapishi ya kambi

a. **Kuchemsha (Simmering)**: hii ni njia ya kuweza kupika chakula kwa kutumia maji na pasipo kukiunguza. Vyakula pendekezwa kwa njia hii ni viazi, maharage, mboga zilizokaushwa n.k.

Namna ya kupika

- Chukua chungu chako na uweke maji ya kutosha
- Weka chakula chako ndani ya maji
- Weka motoni mpaka maji yachemke kabisa
- Baada ya maji kuchemka punguza moto wako, au inua chungu chako juu

18

## Mapishi ya kambi

**b. Mkate kwenye kijiti (Bread on a stick);**

- Andaa unga wako vema
- Chukua kijiti chenye urefu wa sentimita 100 – 130
- Ondoa ganda la kijiti chako na kisha kikaushe vema juu ya moto
- Zungusha kikando chako kwenye fimbo pasipo kuacha nafasi
- Hakikisha unaacha sehemu ya kushikia kama sm15 hivi
- Shika kijiti chako na uanze kuzungusha taratibu juu ya makaa yawakayo
- Endelea kufanya hivyo hadi mkate wako ugeuke rangi na kuwa kama brown hivi, hapo mkate wako utakuwa tayari kwa kuliwa
- Kula mkate wako ukiwa hapo hapo katika kijiti
- Ni vema kufanya zoezi hili wakati wa asubuhi ambapo kila mtu anatamani kuupa mwili wake joto, aua wakati wa usiku manapokuwa mmeuzunguka moto

19

## Mapishi ya kambi

**c. Kuoka kwa aluminium foil (Aluminum foil baking):** njia hii hutumika kupika vitu mbalimbali kama vile viazi vilivyokatwakatwa, mboga majani, ugali n.k.

- Chukua aluminium foil na kisha weka juu yake chakula unachotaka kupika
- Hakikisha chakula chako kinawekwa kwa namna ya ubapa ili kukifanya kiive chote kwa pamoja
- Ifunge Aluminum foil yako vema na kisha ifukie chini ya makaa ya moto yawakayo vizuri
- Kwa chakula kama viazi, ndizi, bisi, ugali acha viive kwa dakika 15 – 20 ndipo unaweza kujithibitishia ikiwa vimeiva au la
- Ikiwa viko tayari basi waweza kula.

20

## Mapishi ya kambi

**d. Yai kwenye ganda la chungwa au kitunguu**

- Chukua chungwa na kisha ulikate katikati na utoe nyama yake ya ndani pasipo kuharibu ganda lake
- Ikiwa utatumia ganda la kitunguu, kata kitunguu chako kutoka juu mpaka jinni, tenganisha kitunguu chako na uchukue tabaka moja la kitunguu lililojaa majimaji
- Hakikisha ganda lako la kitunguu au chungwa lina muundo kama wa bakuli zuri
- Pasua, koroga na uweke chumvi kwenye yai lako likiwa kwenye kikombe
- Chukua kijiti chembamba chenye urefu wa sm90 hadi sm100
- Kichonge vizuri katika ncha yake na kisha kipitishe katikati ya ganda lako kwa uangalifu
- Weka yai lako lililokorogwa vizuri ndani ya ganda hilo na kisha shika kwenye ncha ya kijiti chako
- Weka yai lako juu ya moto huku ukiwa umeshika kijiti chako (hakikisha ganda haligusi moto)
- Fanya hivyo mpaka yai lako litakapokuwa limeiva

21

## Mapishi ya kambi

**e. Yai kwenye jiwe**

- Washa moto wa nyota (star fire) kwa kutumia kuni za ukubwa wa kawaida na si magogo
- Chukua jiwe bapa lililo laini na safi
- Liweke juu ya moto mpaka lipate moto kabisa
- pasua yai lako, likoroge na kuweka chumvi likiwa ndani ya kikombe
- Kisa mimina yai lako juu ya jiwe hila lenye joto
- Ikiwa unapenda kupika jicho la ng'ombe, pasua yai lako moja kwa moja juu ya jiwe la moto
- Yai likiwa tayari, toa jiwe juu ya moto na yai lako litakuwa tayari kwa kuliwa.

22

## Namna ya kutunza chakula katika ubaridi bila kutumia barafu

- Funga chakula kwenye aluminium foil na ukifiche vizuri pembeni mwa kijito
- Chimba shimo usawa wa kiuno au kitovu, kisha tengeneza chumba cha chini katika shimo na uweke huko chakula chako (njia hii hutumika katika maeneo yenye baridi)
- Usitunze chakula katika mahema wanakolala watu, maana kuna Wanyama au wadudu wanaofuata harufu ya chakula hivyo unaweza kusababisha shida kambini
- Ikiwa njia hizo za kutunza chakula zinashindikana ni vema kuning'iniza chakula kwenye matawi ya miti kwa kutengenezea kichanja cha kuning'iniza ai kwa kufunga kwenye wavu au turubai
- Hakikisha vyombo vinayotumika kwa chakula vinakuwa visafi muda wote

23

## Moto katika biblia

- Mwanzo 4:4 – moto ulitumika kwa ajili ya kutoa sadaka
- Mwanzo 19:24 – moto ulitumika kama adhabu kwa wakaidi waliokataa kumtii Mungu
- Kutoka 13:22 – Mungu aliwaongoza Israeli kwa nguzo ya moto wakati wa usiku
- Isaya 44:16 – watu huota moto ili kuipa miili yao joto
- Ufunuo 3:18 – moto hutumika kusafishia vito
- Ufunuo 20:14-15 – dhambi na wadambi watatupwa katika ziwa liwakalo moto na kiberiti, moto huupia utaisafisha dunia yote

24

## Rejea

Retrieved from "https://en.wikibooks.org/w/index.php?title=Adventist_Youth_Honors_Answer_Book/Recreation/Fire_Building_%26_Camp_Cookery&oldid=3251046"

25